

# **Kutengeneza unga wa pilipili**

## **Usindikaji wa pilipili**

Kwa sababu ubora hutegemea matunzo, safisha pilipili na uondoe zilizooza na mashina yoyote ambayo yamebaki kwenye matunda. Kausha pilipili kwenye kikausho hadi usiku kucha huku zikitandazwa kwenye trei. Angalia mara kwa mara kama pilipili zimekauka na ubadilishe vikao vya trei ndani ya kikausho kwa ukaushaji sawa. Pia tandaza pilipili kwenye mkeka safi chini ya jua na uzigeuze kila saa ili ikauke sawa.

Vile vile, zikaushe kwa muda wa siku 5-10 kulingana na hali ya hewa, na saga pilipili hoho kwenye kinu ili kupata unga laini. Acha unga upoe kabisa kabla ya kuweka kwenye chupa. Safisha chupa na zikaushe kabla ya kuweka unga wa pilipili . Funga chupa baada ya kuweka pilipili.

Mwishowe, weka lebo kwenye chupa na tarehe ya kumalizika muda wake.